

MAFUNZO YA KUTUMIA KANZIDATA ZILIZOLUPIWA NA WIZARA KATIKA OFISI ZA HAZINA NDOGO NA WAHAKIKIMALI MIKOANI.

Maktaba ya Wizara ya Fedha na Mipango ipo katika kazi ya kutoa mafunzo kwa Watumishi wote wa Wizara juu ya namna ya kutumia machapisho, majarida na Vitabu vilivyopo kwenye kanzidata zilizolipiwa na Wizara kwa kupitia Shirikisho la Maktaba za Vyuo Vikuu Tanzania (COTUL).

2. Kazi hii yakutoa mafunzo yametokana na maelekezo yaliyotolewa katika kikao cha tarehe 05 Julai 2019 kati ya Watumishi wote wa Wizara na Uongozi wa Wizara ambapo Watumishi waliomba Maktaba ifanye mchakato wa kupata kanzidata zenye vitabu, majarida na Machapisho mbalimbali ili ziweze kuwasaidia katika kazi zao za kila siku.
3. Baada ya Menejimenti ya Wizara kujiridhisha na kuridhia kwamba kanzidata hizi zianze kutumika, Maktaba iliandaa mafunzo kwa ajili ya kuwaelekeza Watumishi jinsi ya kutumia kanzidata Pamoja na kupatiwa nywila (*Password* na *Username*) ili waweze kutumia kanzidata hizo wakiwa nje ya miundo mbinu ya Wizara.
4. Awamu ya kwanza ya mafunzo yameshafanyika ambapo Watumishi wa Wizara ya Fedha na Mipango walifundishwa jinsi ya kutumia kanzidata Pamoja na kupatiwa nywila (*Password* na *Username*) ili waweze kutumia kanzidata hizo wakiwa nje ya miundombinu ya wizara.
5. Aidha, Awamu ya pili ya mafunzo yameshafanyika ambapo Watumishi wa Ofisi za Hazina Ndogo na wahakikimali Mikoani walifundishwa jinsi ya kutumia kanzidata Pamoja na kupatiwa nywila (*Password* na *Username*) ili waweze kutumia kanzidata hizo wakiwa nje ya miundombinu ya wizara, Mikoa iliyofanyiwa mafunzo hayo ni Morogoro, Pwani, Dar-es-salaam, Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Singida, Mwanza, Shinyanga, Simiyu, Geita.
6. Awamu ya Tatu ya Mafunzo yatafanyika katika mikoa ifuatayo ni: **Kagera, Kigoma, Tabora, Singida, Iringa, Njombe, Mbeya, Rukwa, Ruvuma, Mtwara, Katavi, Lindi na Songwe.**
6. Ratiba ya Mafunzo imeambatanishwa.

NO	OFISI YA HAZINA NDOGO NA WAHAKIKIMALI MIKOANI	TAREHE
1	Tabora	8,9 na 10 Novemba 2021
2	Kagera	11, 15 na 16 Novemba, 2021
3	Mara	17,18 na19 Novemba, 2021
4	Njombe	22,23 na 24 Novemba, 2021
5	Iringa	25,26 na 29 Novemba 2021
6	Kigoma	30 Nov, 1 na 2 Disemba, 2021
7	Katavi	3,6 na 7 Disemba, 2021
8	Mbeya	8,9 na 10 Disemba, 2021
9	Songwe	13,14 na 15 Disemba, 2021
10	Rukwa	16,17na 18 Disemba, 2021
11	Ruvuma	20,21 na 22 Disemba, 2021
12	Mtwara	23,27 na 28 Disemba, 2021
13	Lindi	29,30 na 31 Disemba, 2021